# SIRI ZA BIASHARA

## Kwa Ajili Ya Kuzidisha-Mapato




**10X**

**Mwongozo Kamili Wa Kupata Wateja Na Kukuza Biashara Yako**

**VIANNEY MAHIMBI**

Grandimasta

# SiRI
## ZA BIASHARA
### Kwa Ajili Ya Kuzidisha-Mapato

Kimeandikwa na kusanifiwa na:

**VIANNEY E.M. MAHIMBI**

**NUNUA KITABU**

# “Nikisoma kitabu hiki nitapata nini?”

**10X**

**Mwongozo Kamili Wa Kupata Wateja Na Kukuza Biashara Yako**

**… pamoja na siri za biashara ambazo hujawahi kuzisikia mahali popote duniani.**

© 2020 Vianney E. M. Mahimbi
Haki zote zimehifadhiwa

# Dedikasio

**Kitabu hiki cha kiugunduzi kinatolewa kwa heshima ya watuwote ambao wanataka kutumia nguvu ya "biashara" kufanya vitu vya maana hapa duniani.**

# SIRI ZA BIASHARA NI KITU GANI?

## Katika kitabu hiki, tunaposema "SIRI ZA BIASHARA" tunamaanisha:

- ✓ Mikakati
- ✓ Mbinu za masoko
- ✓ Fomla za kutengeneza pesa
- ✓ Na miongozo ya kusimamia biashara ambayo inafanya kazi kwa pamoja kama mfumo.

Kwa hiyo...

SIRI ZA BIASHARA ni mfumo wa kuzidisha-mapato.

Tumia mfumo huu wa kipekee kutengeneza biashara uliyokuwa unatamani kumiliki. Biashara ambayo inakuingizia pesa nyingi na faida kubwa. Hii ndiyo biashara unayostahili kumiliki. **Bofya hapa ujipatie nakala yako!**



# KITABU CHA SIRI ZA BIASHARA

**Ndani ya kitabu hiki kuna mwongozo kamili wa kupata wateja na kukuza biashara yako. Mwongozo huu umegawanyika katika sehemu tatu:**

SEHEMU YA KWANZA

----------------

**ZUNGUMZA LUGHAMOJA NA WATEJA NA WATAKUPATIA CHOCHOTE UNACHOTAKA**

SEHEMU YA PILI

----------------

## ULENGAJISOKO

**Jifunze kulengasoko ambalo litakupatia mapato ya uhakika na faida kubwa**



SEHEMU YA TATU

----------------

**MPANGO WA KUZIDISHA-MAPATO**

**- Zote ndani ya kitabu kimoja -**

## Pamoja na “BONASI” mbili za nguvu

1. Jinsi ya Kutumia Mitandao ya Kijamii Kukuza Biashara Yako.
2. Siri ya kutawala soko la bidhaa zako bila ushindani

**NUNUA KITABU**

# KWANINI UNAHITAJI
## MFUMO WA KUZIDISHA-MAPATO

Katika ulimwengu wa biashara, mapato ni kama *oksijeni.*

Kila mtu anayemiliki biashara anahitaji mapato. Ukiwa na uwezo wa kuzidisha mapato, utapata pesa za kutosha kukuza biashara yako, kuishi maisha mazuri na kutimiza malengo yako.

Lakini wengi tunashindwa kuongeza mapato kwa sababu tunafanya biashara kwa kubahatisha. Na kwa sababu hatuna mwongozo, tunafanya kosa la kutawanya pesa na juhudi zetu huku na kule bila manufaa yoyote. Lakini usijali.

KITABU CHA SIRI ZA BIASHARA kinakupatia “mwongozo kamili” wa kupata wateja na kukuza biashara yako. Wamiliki wa biashara za kila aina tayari wanatumia mwongozo huu kuzidisha-mapato. Na wajasiriamali wote wanaotamani kutengeneza pesa nyingi wanakipenda kitabu hiki kwa sababu:

SIRI ZA BIASHARA ni mkusanyiko wa mikakati na fomla za kutengeneza pesa ambazo zinafanya kazi kwa pamoja kama **Mfumo wa Kuzidisha-Mapato.**

Mfumo huu ni mwongozo kamili wa kupata wateja na kukuza biashara yako.

Kama ukifuata mwongozo (ambao tunakupatia katika kitabu hiki), utakuwa na mfumo wa kukuza biashara yako bila kupoteza pesa wala juhudi zako kwenye mbinu za kubahatisha. Badala yake, utaepuka kufanya makosa ambayo yanawatesa wajasiriamali wengi.

Kitabu hiki kinakupatia mikakati na fomla ambazo makampuni makubwa wanatumia kutengeneza pesa na faida. Lakini tumezipangilia fomla hizo ili uweze kuzitumia kama mfumo wa kuzidisha mapato.

Ukitumia mfumo wetu wa SIRI ZA BIASHARA, unakuwa na uwezo mkubwa kuliko wasomi wengi ambao wanahangaika kukuza biashara kwa kubahatisha.

Kwa hiyo, tumia kitabu hiki kama mfumo unaokuwezesha kuzidisha mapato na faida. Kitabu hiki kimewapatia mwongozo watu wengi na kuwasaidia kutengeneza biashara za nguvu. Naamini kitakusaidia na wewe kumiliki biashara ambayo umekuwa ukitamani kumiliki. Biashara inayokupatia mapato na faida kubwa.

Nakutakia usomaji mwema!

# ZIDISHA-MAPATO MARA 10 NA ZAIDI…

Ndani ya kitabu hiki kuna fomla ya kuzidisha-mapato ya biashara yako mara 10 na zaidi…

Watu wengi tayari wanatumia fomla hii kwa sababu ni nyepesi kuliko unavyofikiri.

**Angalia! Unazungumza LughaMoja na mteja wa kwanza. Baada ya kufanya naye biashara, unamshika kisawasawa. Na kisha unafanya vivyo hivyo kwa wateja wengine 10. Hapa tayari umezidisha mapato yako mara 10. Unaona ilivyo *simpo.* Ni kama vile unawapiga fotokopi wateja wako.**




Lakini kama ambavyo huwezi kupiga fotokopi makaratasi bila kuwa na mashine, ndivyo ambavyo huwezi kuzidisha idadi ya wateja au bidhaa unazozuza bila kuwa na fomla ambazo unaweza kuzirudia tena na tena. Mfumo huo wa fomla za kuzidisha-mapato unaitwa SIRI ZA BIASHARA.

Unahitaji mfumo wa aina hii, ili kuwa na mwendelezo.

Kama unatumia mbinu za kubahatisha, hutaweza kuzidisha idadi ya wateja wala mauzo kwa sababu kila siku ni kama vile unaanza upya.

Kufanya biashara kwa kubahatisha ni adui wa biashara endelevu. Unaenda kwa mteja wa kwanza unamwambia hiki. Mteja mwingine unamwambia kile. Hauna mwendelezo. Unajaribu ututiri wa mbinu kwa sababu hauna mwongozo unaokuwezesha kuchagua njia sahihi ya kukuza biashara yako.

## EPUKA MBINU ZA KUBAHATISHA

Wasomi wengi na wataalamu wa biashara wanatufundisha mbinu nyingi za kutafuta wateja huku na kule. Lakini bila kuwa na mfumo unaounganisha mbinu hizo, hatuwezi kufika popote.

KITABU CHA SIRI ZA BIASHARA kinakupatia fomla na mikakati inayofanya kazi kwa pamoja kama mfumo wa kuzidisha-mapato.

Na kabla hujamaliza kurasa za kitabu hiki, utaweza kutumia mfumo huu kuzidisha-mapato ya biashara yako mara 10 na zaidi…

Unaanza na mteja mmoja. Halafu unatumia fomla hiyo hiyo kupata wateja wengine 10. Na kisha unaongeza idadi yao na kuwa 100. Halafu 1000. Na kuendelea. Hii ndiyo raha ya kutumia **Mfumo wa Kuzungumza LughaMoja Na Wateja.**

## NJIA SAHIHI YA KUKUZA BIASHARA

Mfumo wa Kuzidisha-Mapato ni njia mpya ya kupata wateja na kukuza biashara yako.

Huu ni mwongozo kamili ambao umegawanyika katika sehemu kuu tatu:

1. Mfumo wa Kuzungumza LughaMoja Na Wateja
2. Mpango wa Kuzidisha-Mapato
3. Fomla ya Kuchochea Kasi ya Mafanikio na Ufanisi

Ukifuata mwongozo huu, unapata nguvu ya kuzidisha-mapato kwa sababu sehemu hizi tatu zinafanya kazi kwa pamoja kama mfumo. Kila sehemu ya kitabu hiki imeunganishwa na nyingine ili kukupatia mwongozo kamili wa kupata wateja. Hii ni njia sahihi ya kukuza biashara.

Kama utatumia njia hii kama ninavyoelekeza katika kitabu hiki, utakuwa tofauti na asilimia 99 ya wamiliki wa biashara ambao bado wanatumia mbinu za kubahatisha. Lakini kabla ya hapo, tunajibu swali hili…

# KWANINI NIMEANDIKA KITABU AMBACHO KINAKUFICHULIA SIRI ZA BIASHARA

## Nilianza kujifunza siri za biashara takribani miaka 15 iliyopita. Nakumbuka, ilikuwa hivi…

Baada ya kuhitimu chuo kikuu, nilianzisha biashara binafsi. Licha ya kwamba nilikuwa na bidhaa nzuri, sikuweza kupata mteja hata moja. Watu wakasema nina roho ya kukataliwa. Wengine walinicheka. Wengine wakasema nina mikosi ndiyo maana kila nachojaribu nafeli. Wengine wakasema bidhaa zangu zinakataliwa kwa sababu sijui kuzungumza LughaMoja na wateja. Niliumia sana. Lakini, sikukata tamaa.

Ukweli unauma, lakini unasaidia. Ni kweli nina bidhaa nzuri, lakini sitaweza kuuza chochote mpaka nijifunze kuzungumza LughaMoja na wateja. Bila kutumia ujumbe wa biashara ambao wateja wanaupenda, bidhaa zangu zitaendelea kudoda sokoni. Nashukuru kugundua ukweli huu.

Tangu siku hiyo, nikaanza kujifunza siri za biashara, mbinu za masoko, mikakati ya kuzidisha mapato na fomla za mauzo. Nilinunua kila aina ya vitabu vinavyofundisha mbinu za masoko, siri za biashara, fomla za kuzidisha-mapato na fomla za mauzo.

Nilijifunza kwa bidii mpaka kuna taasisi wakanitunuku cheti cha kuwa mtaalamu wa masoko niliyeidhinishwa. Watu wengi walinipongeza, lakini binafsi niliona ni kitu cha ziada kwa sababu sikujifunza mbinu za masoko ili nipate cheti au Beji ya Kimataifa. Nilijifunza mbinu za masoko ili niweze kuzidisha mapato ya biashara yangu. Kwa hiyo, niliendelea kuzijaribu na kuzifanyia marekebisho mbinu zote nilizojifunza ili ziendane na mazingira yetu.

Na sababu hakukuwa na wataalamu wanaojua siri za biashara, kuna wamiliki wa makampuni wakaomba niwasaidie kutengeneza mifumo ya kuzidisha mapato. Kampuni ya kwanza walinilipa dola za kimarekani 4500 (kama shilingi milioni 10 hivi za kitanzania). Kusema kweli, nilifurahi sana kutumia siri za biashara kuwasaidia wamiliki wa makampuni kuzidisha mapato.

Lakini ghafla, nikapata tatizo lingine.

**Watu wengi walikuwa  wanapenda kujifunza siri ninazotumia kuzidisha-mapato. Lakini kulikuwa na vikwazo viwili:**

1. Kwanza, nilikuwa nafanya kazi na kampuni moja  tu mpaka nimalize programu ya kuzidisha-mapato. Kwa hiyo, sikuwa na muda wa kuwasaidia wamiliki wengine wa biashara.
2. Lakini mbaya zaidi, wajasiriamali wa kawaida walikuwa hawana bajeti ya shilingi milioni 10 kwa ajili ya kuendesha Programu ya Kuzidisha-Mapato.

Tatizo hili liliniumiza sana kwa sababu watu wengi wanaoteseka kufanya biashara kwa kubahatisha ni ndugu zangu. Wengine ni rafiki zangu. Wengine wanapoteza mitaji. Wengine biashara ikiwa mbaya wanachanganyikiwa. Wengine ni wahitimu wa chuo kikuu ambao hawajui wapi pa kuanzia. Wengine wakikataliwa na wateja, wanakata tamaa na kuchukia kufanya biashara.

Haiwezekani. Siwezi kuwaacha watuwote hawa waendelee kupata mateso ambayo niliteseka nilipokuwa sijui siri za biashara.

Kwa hiyo, nikakusanya uzoefu wangu wote, ujuzi nilionao, mafunzo niliyopitia (hasa changamoto za mtaani), vitabu nilivyosoma na fomla zote ambazo huwa natumia kuzidisha mapato ---- na kisha nikatengeneza KITABU CHA SIRI ZA BIASHARA. Kitabu hiki kinakuwezesha kuzidisha-mapato kwa kufanya mambo matatu:

1. Zungumza LughaMoja na Wateja na Watakupatia Chochote Unachotaka
2. Lengasoko Ambalo Linakupatia Mapato Na Faida Kubwa
3. Tengeneza Mpango wa Kuzidisha-Mapato

Naamini kitabu hiki kitawapatia mwongozo watuwote wanaohitaji kupata pesa, lakini hawana muda wa kuchunguza siri za biashara kwa miaka 15 au wamekosa bajeti ya kuajiri wataalamu wa masoko wenye mifumo ya kuzidisha-mapato.

Na hapa ndipo unapoingia.

Kitabu hiki kitakufundisha kuzungumza LughaMoja na wateja wako na kubadilisha jinsi unavyofanya biashara. Kwa hiyo, kipokee kitabu cha SIRI ZA BIASHARA kama mshirika wako mkuu na kitakusaidia kuzidisha-mapato mpaka utashangaa.

## ILI KUNUFAIKA ZAIDI NA KITABU HIKI

Nasisitiza ufanye mambo manne:

1. Chagua biashara au bidhaa ambayo unataka kuzidisha-mapato
2. Soma kila sura na kuelewa jinsi ya kutumia siri za biashara
3. Jaza templeti na majedwali katika sura unayosoma
4. Anza kutumia mpango wako wa kuzidisha-mapato

Ukifuata mwongozo huu, nakuhakikishia, utakuwa na mfumo wa kukuza biashara ambao utautumia maisha yako yote. Na mimi nitafuatilia vyombo vya habari kusikia jinsi biashara yako inavyofanya mambo makubwa katika jamii na kuchochea ukuaji wa uchumi.

Lakini ili upate haya yote, kuna jambo tu la kufanya:

**NUNUA KITABU**

Baada ya kujipatia nakala yako, sasa shughuli ni moja tu:
**ZIDISHA – MAPATO MARA 10 NA ZAIDI…**

Hii ndiyo shughuli kuu tutakayokamilisha katika kitabu hiki cha kwanza kuandikwa katika historia ya vitabu vya biashara duniani.

Kwa kusoma kitabu hiki, naamini utazidi kufanikiwa zaidi na zaidi…

*Mfanikishaji wako,*

Vianney Mahimbi
Mwandishi, SIRI ZA BIASHARA

# YALIYOMO

## Kusudi

Kwanini Unahitaji Mfumo wa Kuzidisha-Mapato 7

## Utangulizi

Zidisha—Mapato Mara 10 Na Zaidi 8

## Sehemu Ya Kwanza 16

## ZUNGUMZA LUGHAMOJA NA WATEJA NA WATAKUPATIA CHOCHOTE UNACHOTAKA

### Sura ya kwanza

Jinsi ya Kutumia Nguvu ya Maneno Kuzidisha-Mapato Ya Biashara Yako 17

### Sura ya pili

Kabla Dakika 5 Hazijaisha… Utaanza Kuzungumza LughaMoja Na Mteja Wako wa Kwanza 22

### Sura ya tatu

Watu Wasipokiona "Kitu Hiki" Wanakataa Kununua Bidhaa Zako 27

### Sura ya nne

Walinicheka Nilipowaambia Nimegundua Siri Ya Kuzungumza LughaMoja Na Wateja – Lakini Nilipowaonesha Fomla Hii 32

## Sehemu Ya Pili 46

# ULENGAJISOKO

### Sura ya tano

Swali Hili la Kitoto Litakusaidia Kulengasoko Na Kuokoa Shilingi 2, 000, 000.00 Na Zaidi 47

### Sura ya sita

Fomla ya Kupata Wateja Bila Kufanya Matangazo ya Biashara 52

### Sura ya saba

Jinsi ya Kulenga Soko 57

### Sura ya nane

Sasa Upo Tayari Kuzidisha Mapato 70

## Sehemu Ya Tatu 72

# MPANGO WA KUZIDISHA-MAPATO

## [Ni Ukurasa Mmoja Tu, Lakini…]

### Sura ya tisa

Kwanza Kabisa, Cheza Na Vitu Viwili 73

### Sura ya kumi

Fomla ya Kuzidisha-Mapato kwa Kutumia Maneno 12 Tu! 76

## Sura ya kumi na moja
Jinsi ya Kutengeneza Malengo Ambayo Yanakuhamasisha Kuzidisha-Mapato 80

## Sura ya kumi na mbili
Jinsi ya Kuhakiki Lengo Lako Kwa Kutumia Vitu Vitano 87

## Sura ya kumi na tatu
Njia-7 za Kuzidisha Mapato 89

## Sura ya kumi na nne
Huu Hapa! Mpango wa Kuzidisha Mapato 109

## Sura ya kumi na tano
Zidisha-Mapato Kila Siku 111

Sehemu Ya Nyongeza 118

# ZIDISHA-MAPATO KILA SIKU

## Sura ya Nyongeza 16
Jinsi ya Kutumia Mitandao ya Kijamii Kuzidisha-Mapato 119

## Sura ya Nyongeza 17
Kifaa cha Siri: Fanya Mapinduzi Kwenye Soko na Utazidisha Mapato Mara Nyingi Upendavyo 131

**18** Shukrani 144

**19** Nukuu 144

**20** Kuhusu Mwandishi 145


**NUNUA KITABU**

## SEHEMU YA KWANZA

# ZUNGUMZA "LUGHAMOJA NA WATEJA" NA WATAKUPATIA CHOCHOTE UNACHOTAKA

"

Bila kujua nguvu ya maneno, huwezi kuwajua watu

**-- CONFUCIUS**

*Sura ya kwanza*

# JINSI YA KUTUMIA “NGUVU YA MANENO” KUZIDISHA-MAPATO YA BIASHARA YAKO

Kila mjasiriamali anataka kuzidisha mapato. Hili ni lengo namba #1 na muhimu kuliko yote katika biashara. Na sababu ipo wazi.

Ukiwa na mapato una uhakika wa kuendesha biashara yako bila wasiwasi. Unalipa mishahara kwa wakati. Unapata faida. Unalipa kodi na kutunza familia vizuri. Unafurahia maisha. Na bado unabakiwa na pesa kwa ajili ya kufanikisha malengo yako mengine. Kwa sababu hii, kila mmiliki wa biashara anataka kuzidisha mapato.

Lakini bahati mbaya, lengo lako la kutengeneza faida halina maana yoyote kwa mteja. **Biashara yako ni biashara yako!**

Suala la kuzidisha mapato na kukuza biashara yako siyo kipaumbele cha mteja hata kidogo.  Unataka kuzidisha mapato, mteja anataka kuokoa pesa. Hili ni tatizo kubwa!


Lakini usijali. Ndani ya kitabu hiki utajifunza mfumo wa kuzungumza LughaMoja na wateja. Ndiyo!

Hii ni  njia mpya ya kuzidisha mapato katika karne ya 21.

Lakini kabla sijakueleza jinsi ya kutumia ugunduzi huu kukuza biashara yako, kuna jambo nataka kukushirikisha. Na jambo lenyewe ni hili…

Mwisho wa sampo (Bofya hapo chini)

# NUNUA KITABU






NUNUA KITABU